

Aprili 22, 2020

Wapendwa Familia za JCPS,

Hatuwezi kueleza jinsi tumefurahishwa na matokeo ya wiki mbili na nusi za kwanza za kusomea nyumbani. Wiki iliyopita, asilimia 93 ya karibu wanafunzi 100,000 wa JCPS walishiriki katika Masomo Yasiyo ya Kiasili(NTI) na walimu wao. Hata kuns shule zingine waliokuwa na ushirika wa aslimia 100. Hizo ni idadi za kushangaza! Ni agano kwa wazazi wetu, walezi, familia, wanafunzi na walimu ya kwamba tunatafuta kuhusika kwa aina hii kwa shule chini ya nyakati ngumu hivi. Asante kila mmoja wenu.

Tunazo habari zingine za kushiriki nanyi:

- **Siku ya mwisho ya shule kwa wanafunzi wa JCPS sasa imepangwa kuwa mnamo Mai 27.** Bodi ya Elimu ya Kaunti ya Jefferson ilikubali mabadiliko kutoka Juni 3 hadi Mai 27 katika mkutano wa jana usiku. Wanafunzi watakamilisha kilichobaki cha mwaka wa shule kupitia NTI. Kuna uwezekano tutaona wilaya ndogo za shule kadhaa na za kibinafsi na za kibarokia zikimaliza kabla ya JCPS. Wengi wao walianza kusomea nyumbani mnamo Machi 16 wakati JCPS ilihitaji wiki mbili kuunda mfumo wake wa NTI na kuhakikisha kila mwanafunzi ana ufikiaji wa kompyuta, tatizo ambalo wilaya nyingi hawakulazimika kupambana nalo. Tunaamini ulikuwa ni wakati uliotumiwa vizuri, huku ukitoa mazoea ya kielimu kwa wanafunzi wetu WOTE.
- **Vifurushi vya Bidhaa za Kielimu:** Vifurushi vilivyo na nakala zilizochapishwa za bidhaa za kieleimu hazitapatikana tena katika kila kiwanda cha Kusambaza Chakula. Kuanzia Ijumaa, Aprili 24, vifurushi vitapatikana katika viwanda 14: Shule za Msingi za Blue Lick, Brandeis, Chancey, Crums Lane, Engelhard, Fern Creek, Frayser, Indian Trail, McFerran, St. Matthews na Wheatley; Shule ya Kati ya Carrithers; na Shule ya Upili ya Valley High na Kituo cha Jamii cha Americana. Tumeanza kutuma vifurushi zaidi moja kwa moja kwa wanafunzi ili kupunguza haja ya kuwa na viwanda vingi vya kuchukulia.
- **Onyeshana Mtoto Wako:** Tafadhali tuonyeshe jinsi mtoto wako anafanya NTI nyumbani. Unaweza kuweka video fupi au picha kwenye mitandao ya kijamii na ujumuishe alama za reli #ThisIsHowINTI na #WeAreJCPSAtHome au unaweza kuzituma kwetu kwa jcps.communications@jefferson.kyschools.us.

Tunajua wengi wenu wanajitenga kijami, kufanyia kazi nyumbani na pia kusaidia mtoto wako na kazi yake ya shule. Tunaelewa. Jitahidi tu. Walimu, wasimamizi na wafanyikazi katika JCPS wanafanya vivyo hivyo. Tuko hapa kusaidia wewe na mtoto wako wakati huu usiokuwa umetarajiwa katika historia ya Marekani.

Kwa dhati,

Mawasiliano ya JCPS